KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 12, Issue 2

7th SHA'BAAN 1432

8th July, 2011

YALIYOMO

MWEZI WA ALMASI 1 - 2

NASWAHA YA RAMADHAAN 2 - 4

MWEZI WA ALMASI

Sheikh Muhammad Kasim Mazrui (رحمه الله)

[*Yafuatayo ni makala ya Sheikh wetu Muhammad Kasim Mazrui* (رحمه الله)]

Imehadithiwa kwamba katika jimbo fulani la Ulimwengu kulikuwa na mfalme karimu sana, mwenye busara kubwa, na mwenye hima ya kuamirisha dola yake na kutunga maslaha ya raia zake. Mfalme huyo aligundua ardhi moja kubwa iliyojaa almasi katika jimbo lililokuwa tini ya ufalme wake. akaikatakata ardhi ile vipande kadha wa kadha, na akatangaza kuwa yoyote katika raiya zake atakaekutimba almasi, yuko tayari kumpa kipande katika ardhi hiyo atimbe almasi. Kila mmoja katika raiya akajifunga na kujizatiti kwenda na kuomba apewe kipande ili ajipatie utajiri. Walipofika mbele ya mfalme akawapa amri killa mmoja atukuwe kipande atakacho, afanye kazi kwa muda wa siku thelathini; almasi atakayopata katika muda huo ndio yake. Baada ya hapo watapokonywa wao wapawe wengine. Killa mtu akatukuwa kipande atakacho na kazi ikaanza.

Killa mmoja akifanya jitihada apate almasi nyingi kadri atakayoweza siku thelathini zikisha nae awe amekwisha tajirika. Waliokuwa na hima katika wao walikuwa wakifanya kazi usiku na mtana. Hawali illa kadri ya kuondoa ndaa wala hawalali illa kadri ya kujipumzisha, nyakati zao zote wakazitumia katika kufanya kazi. Siku thelathini zilipofika, nao walikuwa wamekwisha tajirika, wakatukuza almasi yao kwa furaha huku wakimshukuru mfalme wao ambae wakati huo yeye na watumishi wake walikuwa wamesimama penye roshani ya jumba lake wakiwatazama na kuwapa heko kwa hima yao na kufaulu kwao.

Wengine hawakuwa na hima kama hiyo. Walifanya kazi katika nyakati za kazi tu kama wafanyavyo maofisi. Asubuhi walikuwa kwanza wakitengeza chai ya nguvu, wakajipiga barabara, ndipo watokapo kwenda kazini. Ikipata saa nne wakapumzika na kunwa chai kidogo. Adhuhuri wakaata kazi, na kuingia kuandalia pilau nzuri na namna-namna za vitoweo. Wakishapakia ndipo waendapo kazini. Ikifika saa kumi kukafumuliwa machai na makeki. Kisha killa mmoja akaenda kutembea au kutaanasi kwa anasa yake, kazi mpaka kesho. Na kwa sababu ya kula sana, hawakuwa na uchachamavu wa kutosha katika kazi yao, na wengine wakawa mara kwa mara huzukwa ni matumbo wakaata kazi na kukimbilia chooni. Siku thelathini zilipomalizika wakajiona hawakupata illa kadri ya gharama walizotumia katika timbo. Walipokwenda kwa mfalme kutoa shukrani zao, wakamuonyesha almasi waliyopata, mfalme alisukasuka kitwa kwa masikitiko na huku akiwaambia, "kama killa siku mngekuwa mkikumbuka kuwa siku zenu ni thelathini tu, mungetumia nyakati zenu katika kufanya kazi, mukaata kujishughulisha kwa kula na kustarehe, mungepata kama walivyopata wenzenu". Wakaondoka nan huzuni na majuto wakaenda zao.

Tapo la tatu, walipotoka kwenda huko kwenye timbo, walitukuwa vifaa na ala zote za kustarehea, hatta wanawake pia! Kufika hapo kiwandani kwanza walitandika majamvi wakateza karata! Wakisha hawa wakaja hawa! Saa zawapitia hawana khabari! Walipouchoka mtezo wa karata wakaingilia mwengine na hivyo hivyo. Walipochoka kuteza ikawa ni wakati wa kuandalia chakula. Kukafumka mabiriani na vinwewa tamu tamu, wakala hatta pumzi zikawa juu-juu! Baada ya muda mchache usingizi ukawashika wakajibwaga juu ya majamvi na kulala kama magogo! Hawakuzindukana illa jioni. Wakaingia kutengeza machai ya alasiri na vyakula vya usiku. Usiku, baada ya chakula, wapigaji muziki walikuwa tayari, ikauma dansi mpaka karibu na alfajiri! Hapo killa mmoja akawa taabani, wakalala wote baada ya kuagana kuwa waanze kazi kesho. Hawakujifahamu illa saa tano za mtana. Kiasi cha kuingia chooni na kujitengeza-tengeza imekuwa saa sita. Wakaona kazi haianziki leo; afadhali tuendelee na starehe zetu mpaka kesho. Lakini kama starehe za jana zilivyowatepeteza kufanya kazi leo, ndivyo starehe za leo zilivyowatepeteza kufanya kazi kesho! Hawakuweza kuata starehe zao hatta siku moja, na kwa hivyo wasiweze

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

kufanya kazi hatta siku moja. Siku thelathini zilipomalizika, killa walichotukua kilikuwa kimemalizika! Mahali pa kupata faida wao wakapata khasara, wakaondoka wakiuma vidole kwa huzuni na majuto. Hali yao ikawaonyesha haya hatta kupita kwa mfalme kutowa shukrani, wakapita ndia za miba na mbiliwili ili mfalme asiwaone!

Huu ndio mfano wa Waislamu na mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao utatuingilia baada ya mwezi mmoja. Jee ndugu Mwislam! Utapenda kuwa katika kumbo gani katika matatu hayo? Utawata upuuzi wako na starehe zako mwezi ukimalizika upate cha kufutia madhambi na akiba njema ya Akhera yako! Au utatangamanisha baina ya amali na upuuzi, mwezi ukisha uwe hukupata illa cha kuzibia pengo za maovu uliyoyafanya! Au utapuuzika uondokee majuto na khasara ya maovu yaliyokugandama shingoni mwako. Hujui kama Ramadhani nyengine utaipata au utakuwa ni katika kumbo la wataoondoka na kuwapisha wajao kama walivyoondoka waliotangulia wakakupisha wewe? Fikiri ni wangapi kama wewe waliondolewa katika mwaka huu. Kwa bahati yako nzuri au mbaya ukaatiliwa usiondolewe pamoja na walioondolewa. Jee, una hakika kuwa bahati hiyo utaipata killa mwaka?! Ikiwa huna hakika — na hakuna mwenye hakika — basi jipinde kutumia nyakati zako zote kufanya kazi ya Mungu katika mwezi huu wa Almasi ili usiondokee majuto. Mungu Atuafikie.

قافلة الرحمة للحج والعمرة Al-Rahma `Umrah & Hajj

Agencies1432 Hijri / 2011 C.E

Assalaamu `Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah Safari yetu ya mwaka huu 1432 Hijri/2011 ya kupeleka watu `Umrah katika mwezi wa Ramadhaan, kumi la mwisho. Na vilevile katika `Ibaadah ya Hijjah.

Mipangilio ya Safari ya `Umrah (Mwezi wa Ramadhaan) ni kama ifuatayo:

• Kuondoka ni tarehe 17 ya mwezi wa Ramadhaan*Kurudi ni baada ya `Eid Insha Allaah

• Safari itaanzia Nairobi – Jeddah

• Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli na Usafiri) ni $1500 U.S

• Siku tatu tutakuwa Madinah na Siku kumi za mwisho tutakuwa Makkah mpaka `Eid.

• Safari ya Kurudi Jeddah – Nairobi. Itakuwa baada ya `Eid

Twapenda kuwahimiza wale wale wenye niya ya kwenda na sisi waharakishe kuleta Passport zao na picha Nne kwa ajili ya kufanya maandalizi. Sababu ni kwamba Viza zitafungwa kabla ya mweizi wa Ramadhaan kuanza.Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa njia zifuatazo:

- Tutumie e-mail katika info@qssea.net au
- Simu nambari +254 723471820 (Abu Bilaal Athman Na'man)
- Simu nambari +254 721473181 (Abu Farida Muhammad Basawad)
- Simu nambari +254 700365253 (Muhammad Abdillaah)
- Simu nambari +254 728653863 (Dr. Ashraf)

Hukmu na Fadhla za Saumu Katika Mwezi wa Ramadhaan.

Sheikh 'Abdul-'Azeez Ibn Baaz

Killa sampuli ya sifa zilizo njema ni zenye kumthubutukia Allaah (سبحانه وتعالى) Peke Yake; Twamuomba autukuze utajo Wake wa Mtume Muhammad, ahli yake na Maswahaba zake wote. Huu ni wasiya mfupi kwa Waislamu wote unaohusiana na kufunga katika mwezi wa Ramadhaan, kuswali kwenye usiku wake, na fadhla za kushindana katika matendo mema katika mwezi huo, kwa kuongezea juu ya hukmu zilizo muhimu ambazo zisizojulikana na baadhi ya watu. Namuomba Allaah atuongoze sisi sote tuwe kwenye njia ya watu walio na Imani, na atuwezeshe sote kuifahamu Qur'an na Sunnah. Imepokewa yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiwapa bishara njema Maswahaba zake pindi uingiapo mwezi wa Ramadhaan. Nae (صلى الله عليه وسلم) alitupasha khabari yakwamba katika mwezi huu milango ya Peponi hufunguliwa, milango ya Motoni hufungwa, na mashetwani hufungwa kwa minyororo. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "*Unapoingia usiku wa kwanza wa mwezi wa Ramadhaan, milango ya Peponi hufunguliwa na milango ya Motoni hufungwa, na mashetwani hufungwa kwa minyororo, na itasemwa, 'Ewe mwenye kutamani kufanya wema! Njoo hapa na Ewe mwenye kutamani maovu! Kaa nyuma', na Allaah ana watu ambao anaowaacha huru na moto katika killa usiku (katika mwezi huo)*." [Al-Bukhaari na Muslim]. Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema akasema, "*Mumejiliwa na mwezi uliobarikiwa, ambao ndani yake Allaah huwakinga nyinyi na Rehma zake, akawasamehe madhambi yenu, akawajibu maombi yenu na akaangalia katika kushindana kwenu kufanya wema na akajigamba mbele ya Malaika wake (kuwahusu watu hao), basi kwahivyo jionyesheni kwa Allaah kutokamana na nafsi zenu katika yale yaliyo mazuri, kwa sababu aliyekosa bahati miongoni mwenu ni yule aliyenyimwa kutokamana na Rehma za Allaah (katika mwezi huu)*." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema, "Yoyote atakaefunga (katika mwezi wa) Ramadhaan kwa Imani, akitarajia

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

malipo mema kutoka kwa Allaah, basi madhambi yake yote kabla ya hapo atasamehewa nayo, na yoyote mwenye kuswali katika (swala za usiku) mwezi wa Ramadhaan kutokana na Imani, akitarajia malipo yatokayo kwa Allaah, basi madhambi yake yote kabla ya hapo atasamehewa nayo."[al-Bukhaari na Muslim].

Katika hadeeth Qudsee, akasimulia kwa niyaba ya Mola wake, "*'Amali zote za mwana wa Aadam huongezwa kwa mara kumi kama malipo yake mpaka mara mia saba, isipokuwa Saumu; hiyo ni yangu Mimi na Mimi ndiye Nitakaeilipa [kama itakavyowajibika], kwani yeye (mwenye kufunga) aliyawacha matamaniwa yake, chakula chake na kinywaji chake (kwa utakaso) kwa ajili yangu.*"

Pia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema*:* "*Mwenye kufunga ana mara mbili za kufurahi, moja wakati atakapofungua saumu yake, na moja ni atakapoonana na Mola wake. Naapa kwa yule ambae mikononi mwake kuna roho yangu, harufu ya mdomo ya mtu aliyefunga mbele ya Allaah kuliko harufu ya musk*." Kuna riwaya nyingi zenye kuhimiza na kuzifafanua fadhla za kufunga katika mwezi wa Ramadhaan, kuswali katika nyakati zake za usiku, na kufunga kwa ujumla. Mu'min na atumie faida za kuishi kwa muda mrefu mpaka afikiliapo katika mwezi wa Ramadhaan, na akimbilie katika kufanya kheri, na ajitahadhari na ma'asiya, na azidishe juhudi zake katika kutekeleza uwajibu uliowekwa na Allaah, haswa swala tano za killa siku, kwani hizo ni kama Uti wa mgongo wa Uislamu na ni uwajibikaji ulio mkubwa zaidi baada ya Shahada mbili za Imani [Shahaadatayn]. Kwahivyo, killa Muislamu, mume na mke, na wazihifadhi swala zao na wazitekeleze kwa nyakati zake zilizowekwa, kwa unyenyekevu na utulivu. Mojawapo ya uwajibikaji ulio muhimu kwa wanaume ni kuzitekeleza hizi swala za waajib kwa jamaa katika misikiti kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى) [kulingana na tafsiri]: **"Na simamisheni swala na toeni zaka na inameni pamoja na wanaoinama (kwa ibada)** [al-Baqarah (2): 43] Akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى) [kama ilivyofasiriwa]: **"Angalieni sana swala (tano za faradhi). Na haswa ile swala ya kati na kati. Na simameni kwa unyenyekevu katika kumwabudu Allaah."** [al-Baqarah (2): 238]

Katika aya nyengine Allaah (سبحانه وتعالى) amesema [kama ilivyo kwenye tafsiri]: **"Hakika wamefuzu Waislamu. Ambao katika swala zao huwa ni wanyenyekevu. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi. Na ambao (nguzo ya) Zaka wanaitekeleza. Na ambao tupu zao wanazilinda. Isipokuwa kwa wake zao au kwa (wanawake) wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, (kulia). Basi hao ndio wasiolaumiwa. (Lakini) anayetaka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka (ya Allaah). Na ambao amana zao na ahadi zao wanaziangalia (wanazitekeleza). Na ambao swala zao wanazihifadhi. Hao ndio warithi. Ambao watarithi Pepo; wakae humo milele.** [Al-Mu'minoon: 1-11]. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم), "*Ahadi iliyoko baina yetu (sisi waumini) na wao (makafiri) ni (hubainishwa kwa kutekeleza) swala, yoyote mwenye kuiwacha, basi atakuwa amekufuru*." (Ahmad).

Uwajibu mwengine wa pili baada ya swala ulio muhimu ni kulipa zaka zilizo wajibu (Zakaah). Allaah (سبحانه وتعالى) amesema [kama ilivyo kwenye tafsiri]: **"Wala hawakuamrishwa illa kumuabudu Allaah kwa kumtakasia Dini, wawache Dini za upotofu, (upotevu) na wasimamishe swala na kutoa Zaka—hiyo ndiyo Dini iliyo sawa.** [Al-Bayyinah: (98): 5). Na pia: **"Na simamisheni swala na toeni Zaka na mtiini Mtume, ili mrehemewe."** [an-Nur (24): 56].

Imedhihiri kutoka katika Qur'n na pia katika Sunnah yakwamba mtu asotoa Zaka ataadhibiwa katika siku ya malipo na mali yake. Ya pili muhimu ifuatayo baada ya uwajibikaji mbili hizi ni kufunga katika mwezi wa Ramadhaan ambao ni mojawapo ya nguzo tano zilizotajwa katika maneno yake Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano*, shahada mbili (za Imani), kusimamisha swala, kufunga, Zakaat ya kuwajibika, na kwenda kuhijji Makkah." [Al-Bukhaari na Muslim]. Muislamu na azilinde ipasavyo saumu yake na swala zake za usiku dhidi ya yale mambo ambayo Allaah aliyoyaharamisha, imma maneno au vitendo, kwa sababu malengo ya kufunga ni kumtwi'i Allaah, na kuyatukuza mipaka yake, kupambana na matamaniwa ya nafsi na haja zake kwa kujizoezesha kustahamili, na kujiepusha na aliyoyakataza Allaah. Kujiepusha na vyakula na vinywaji, na vitu vyengine vyenye kuharibu saumu haikuwa ndilo lengo nyuma ya kufunga. Hiyo ndiyo sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "*Saumu ni kinga, kwahivyo mmoja wenu atakapokuwa amefunga, na asimguse mkewe (kwa mafungamano ya kustarehe), na wala asimtukane mtu yoyote, na iwapo mtu atataka kupigana nae au atamuudhi, yeye na aseme, 'Mimi nimefunga, mimi nimefunga'*"

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Yoyote ambae hatojiepusha na urongo katika maneno yake na vitendo vyake na vitendo vya kijinga (haliyakuwa amefunga), Allaah hana haja na kugomea kwake kula na kunywa." [Al-Bukhaari na Muslim]. Kutokamana na maandishi haya, imedhihirika yakwamba mwenye kufunga na atahadhari na mambo yote yaliyoharamishwa na Allaah wakati anapokuwa amefunga na ajifungamanishe na yote yaliyofaradhishwa. Kama ilivyo matokeo ya haya, inatarajiwa yakwamba Allaah atamsamehe mtu huyo, amuokoe kutokamana na moto na aikubali saumu yake.

MAMBO AMBAYO HAYAJAWAZINDUKIA WATU WENGI

Kuna baadhi ya mambo ambayo watu hawajazindukana nayo au hawayajui. Nayo ni kama yafuatayo:

1Muislamu na afunge kwa Imani peke yake, akiwa na matumaini ya malipo mema kutoka kwa Allaah, sio kwa kujitwaza au kuwaiga wengine katika jamii yake au mji wake. Mambo ambayo yanayotakikana kumpelekea yeye kufunga yanatakiwa yawe ni imani yake yakwamba Allaah amemfaradhishia yeye kufunga na matumanini yake yakwamba Allaah Peke yake ndiye atakaemlipa; vilevile kwa swala za usiku katika mwezi huu, kwa ajili hii Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "*Yoyote mwenye kufunga Ramadhaan kwa Imani na kutarajia malipo ya Allaah, basi madhambi yake yote yaliyopita yatasamehewa, na yoyote mwenyeb kuswali katika mwezi wa Ramadhaan (katika swala za usiku) kwa imani na kutarajia malipo kutoka kwa Allaah, basi*

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

madhambi yake yote yaliyopita yatasamehewa" (al- Bukhaari na Muslim].

2 Hwenda fungaji akapata jaraha, akatokwa na damu zapua, akatapika, au maji yakapita kwenye koo yake kwa bahati mbaya, mambo haya yote hayabatilishi saumu yake, lakini kujitapisha kwa kukusudia huvunja saumu kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "*Yoyote mwenye kutapika pasi na kukusudia, hatokuwa na haja ya kuilipa siku hiyo.*"

3 Baadhi ya wafungaji huwenda wakachelewesha *Ghusl* (josho la janaba) mpaka baada ya mapambazuko ya alfajiri. Kwa mfano, baadhi ya wanawake huwenda wakachelewesha Ghusl baada ya kumaliza ada zao za killa mwezi au damu zao za mazazi mpaka baada ya mapambazuko ya alfajiri iwapo watatanabahi yakwamba wamemaliza damu zao (wakawa tayari kufunga) kabla ya kupambazuka. Katika hali hii, mwanamke huyo itamlazimu kufunga na hapana madhara kwa kuoga kwake baada ya kupambazuka, lakini na asiicheleweshe mpaka baada ya kuchomoza kwa jua kwa sababu ni lazima ajitwahirishe na aswali swala ya alfajiri kabla ya jua kuchomoza. Vilevile, mtu ambae inamlazimu kuoga kwa sababu yeye (mume/mke) alifanya kitendo cha kuundama (kwa mke na mume) na mwenziwe, anaweza kuchelewesha kuoga mpaka baada ya kupambazuka, lakini ni lazima waoge kabla ya kuchomoza kwa jua ili apate kuswali kwa wakati unaofaa. Wanaume ni lazima waharakishe kuoga ili wakaipate swala ya Jamaa.

4 Kupima damu, kudungwa sindano na chanjo ambazo hazikukusudiwa kulisha vyakula haviharibu saumu, lakini iwapo mtu atakuwa na uwezo wa kuvichelewesha mpaka uingiapo usiku, basi hilo litakuwa ni bora. Hii ni kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Wacha (kufanya) jambo ulilo na shaka nalo (katika kuruhusiwa kwake) kwa lile ambalo lisilokusababisha wewe kuwa na shaka (kuruhusiwa kwake).*" Mtume (صلى الله عليه وسلم) pia akasema: "*Mwenye kujiepusha na shubuhaat (mambo yenye shaka)* ameilinda dini yake na heshima yake."

5 Muislamu atakikaniwa awe na utulivu anaposwali; Maandiko mengi yanathibitisha yakwamba utulivu kwenye swala ni miongoni mwa shuruti za swala na kwamba swala ya mtu ikosapo hilo huwa haifai. Utulivu ni kutokimbilia swala, kunyenyekea kwa Allaah na kumakinika katika kila hatua ya swala mpaka kila kiungo na mfupa virudi kwenye sehemu zake za asili. Watu wengi huswali swala ya Taraweeh (swala ya usiku) katika mwezi wa Ramadhaan bila ya kuwa watulivu, na huswali kwa haraka mno mpaka (swala hiyo) ikafanana na kudona kwa Jogoo. Njia kama hiyo ya kutekeleza swala hairuhusiwi, na mwenye kufanya hivyo atakuwa amefanya madhambi.

6 Baadhi ya watu wanadhani yakwamba hawawezi kuswali chini ya rakaa'ah ishirini katika Taraweeh, na wengine hufikiri yakwamba wao hawawezi kuswali zaidi ya rakaa'ah kumi na moja au kumi na tatu. Kuna dalili chungu nzima zenye kuonyesha yakwamba jambo hilo halikufungwa (juu ya idadi maalum) na halina idadi iliyofungwa. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiswali rakaa'ah kumi na moja wakati fulani na wakati mwengine alikuwa akiswali rakaa'ah kumi na tatu, na idadi ndogo ya hizo wakati mwengine. Alipoulizwa (صلى الله عليه وسلم) kuhusu swala ya usiku alisema: "*(Endeleeni kuswali) swala za rakaa'ah mbili mpaka munapohofia yakwamba mapambazuko yamekurubia, kisha mtu anaweza kuswali rakaa'ah moja (witr) kukamilisha swala yake ya usiku kwa hiyo.*" [Bukhaari & Muslim].

7 Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakufunga idadi maalum katika wakati wa Ramadhaan au wakati mwengine, na hiyo ndiyo sababu watu mara nyengine huswali rakaa'ah ishirini na tatu katika zama za 'Umar (رضي الله عنه). Baadhi ya ma-Salaf (رضي الله عنهم) walikuwa wakiswali rakaa'ah thalathini na sita na wakaswali rakaa'ah tatu kama swala ya witr. Wengine waliswali rakaa'ah arubaini na moja, kama ilivyotajwa na Ibn Taymiyyah (رحمه الله) na wanavyuoni wengineo. Amesema Ibn Taymiyyah (رحمه الله) yakwamba suala hilo halikufungwa bali liko wazi na kwamba ni bora kwa awezae kurefusha kisomo chake wakati wa swala na kurefusha ruku' yake na sujood yake kuswali idadi ndogo ya rakaa'ah. Lakini ni bora kwa mtu mwenye kuswali sura ndogo ndogo na kufupisha ruku' yake na sujood yake ili aswali idadi ndogo. Mwenye kuangalia Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) atafahamu yakwamba kuswali rakaa'ah kumi na moja au kumi na tatu ndio njia bora ya kuswali swala za usiku katika mwezi wa Ramadhaan au wakati wowote mwengine. Hii italingana na jinsi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyokuwa akimuabudu Allaah, na njia yake (صلى الله عليه وسلم) ndiyo ya karibu zaidi na utulivu na unyenyekevu wakati wa swala. Ni bora kwa mwenye kuswali pamoja na Imaam wakati wa Ramadhaan, abakie nae mpaka atakapomaliza Imaam, kwa sababu amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Mwenye kuswali swala ya usiku pamoja na Imaam (kwa jamaa) mpaka amalizapo atapata thawabu za kuswali swala ya usiku mzima.*"

8 Imependekezwa kwa Waislamu wajitahidi kadiri ya uwezo wao katika killa aina ya ibada katika mwezi huu, kama vile kusoma Qur'an, kuswali swala za Sunnah.

9 Kumtukuza Allaah, kumshukuru Allaah, kuomba msamaha kutoka kwa Allaah, kumuomba Yeye, kuamrisha mema na kukataza maovu, kuwalingania watu kwa Allaah, kuwasaidia masikini na wenye mahitaji, kuwaheshimu wazazi, kuunga kizazi, kuwa mpole kwa majirani, kuwatembelea wagonjwa na killa aina ya wema kama ilivyo kwenye riwaya iliyotangulia, asema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Allaah huwaangalia katika kushindana kwenu kwa mambo ya kheri, na akajivunia mbele ya Malaika (kuhusiana nayo), kwahivyo jionyesheni kwa Allaah yaliyo mazuri yenu, kwa sababu aliyeharibikiwa ni yule aliyenyimwa Rehma za Allaah.*" Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Yoyote mwenye kufanya amali njema ndani yake (Ramadhaan) atalipwa thawabu za jambo la waajib na yoyote mwenye; na yoyote atakaefanya tendo la waajib la ibada atalipwa mara sabiini zaidi (katika mwezi wa Ramadhaan) kuliko katika mwezi mwengine wowote.*"

Pia imepokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): "'*Umrah katika mwezi wa Ramadhaan, ni sawa na kufanya Hajj (katika malipo).*" Katika riwaya nyengine amesema (صلى الله عليه وسلم): "... *Ni sawa na kufanya Hajj pamoja na mimi (katika malipo).*" Kuna riwaya nyengine nyingi zenye kuthibitisha uhalali wa kushindana katika mas'ala yanayohusiana na wema katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhaan.